

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



Machi 28, 2022

OFISI YA MKUU WA WILAYA,
S.L.P 02,
LUDEWA.

TAARIFA KWA UMMA

**MKUU WA WILAYA YA LUDEWA ANDREA TSERE AKUTANA NA WATUMISHI WA
AFYA WA HOSPITALI YA WILAYA YA LUDEWA**

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere leo Machi 28, 2022 amefanya ziara ya kikazi katika Hospitali ya Wilaya ya Ludewa ambapo katika ziara hiyo aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias.

Katika ziara hiyo Mhe.Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere pamoja na mambo mengine amewapongeza Watumishi wote wa Hospitali hiyo kwa niaba ya watumishi wote wa wizara ya Afya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa kazi kubwa wanayo ifanya kwa kuwahudumia wataanzania kwa weredi na bidii.

Kwaupande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg.Sunday Deogratias amemshukuru Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Ludewa kwa kufanya ziara kwenye Hospitali hiyo na kuona umuhimu wa kuwatia moyo watumishi wote wa idara ya Afya.

Sambamba na hayo akaongeza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiangazia Idara ya Afya huku akitaja kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imepatiwa fedha za ujenzi wa kituo cha Afya Mundindi na Ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi pamoja na nyumba ya watumishi wa Afya.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

Chrispin B.Kalinga
Afisa Habari (W) Ludewa